BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 11 Septemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. KIAPO CHA UAMINIFU:

**Mhe. Chumu Kombo Khamis.**

## II. TAARIFA YA SPIKA:

## III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 28 Juni, 2024.

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## IV. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

231. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari kubwa katika visiwa vikubwa na vidogo vya Unguja na Pemba.

Je, maeneo gani hasa yaliyoathirika zaidi na kuna mkakati gani wa kuyanusuru maeneo yaliyokuwa hayajaathirika na mabadiliko ya tabianchi.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

138. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Historia inatueleza kwamba Wazanzibari tokea zama hizo hadi leo wametawanyika katika mataifa mbali mbali duniani kote.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea mtawanyiko huo.

(b) Ni mataifa gani ambayo yamefanyiwa tathmini na kuaminika kuwa Wazanzibari wapo wengi katika mataifa hayo.

(c) Kwa kiasi gani Wazanzibari waliotawanyika duniani kote wameweza kuitika wito wa kurudi nyumbani kwa ajili ya kuchangia harakati mbali mbali za maendeleo ya nchi yao.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tathmini iko vipi juu ya utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kuwataka wafanyabiashara wadogo wadogo kufanya biashara zao katika maeneo maalumu.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

43. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Tafiti zinaonesha kuwa, katika uchumi wa Afrika vijana watatu kati ya wanne hawana ujuzi wa kushiriki katika uchumi wa kidigitali wa Afrika.

    Je, Wizara ina mikakati gani ya kuona kwamba vijana wanakuwa katika sehemu kubwa ya uchumi huo.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

127. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    (a) Ni nini maana ya sarafu za kielektroniki kwa faida ya wananchi.

    (b) Kwa kiasi gani Serikali inafanya maandalizi ya kutosha ya kuupokea mfumo huu.

    (c) Ni zipi faida zinazotokana na sarafu za kielektroniki.

147. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    (a) Ni yepi mafanikio ya mifumo mipya ya kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha za umma kupitia Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA).

    (b) Kwa kiasi gani changamoto za mifumo hiyo zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo.

**Wizara ya Habari:**

47. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Je, Mabaraza ya Wazee yana mchango gani katika kuhakikisha kwamba mila, silka na utamaduni wetu unarithishwa ipasavyo kwa vizazi vipya.

237. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Serikali ya Awamu ya Nane imefanya kazi nzuri ya kuimarisha miundombinu ya michezo mbali mbali ikiwemo viwanja vya michezo. Hata hivyo, viwanja vya michezo vya Mao Tse -Tung kwa muda sasa vimekuwa katika hali isiyo nzuri.

    Je, Serikali imejipanga vipi kuvifanyia ukarabati mkubwa viwanja hivyo katika bajeti ya mwaka huu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

4. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kudhibiti usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya magendo, bado kuna watu wasio waaminifu wanaoendelea na kujishughulisha na usafirishaji wa bidhaa kwa kutumia bandari zisizo rasmi.

    (a) Je, ni ipi mikakati ya Serikali katika kulitokomeza kabisa suala hili la usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya magendo.

    (b) Ni zipi adhabu zilizowekwa kisheria kwa watu ambao watabainika na kadhia hii.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

56. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Tathmini iko vipi juu ya idadi ya kutosha ya uwepo wa wataalamu wa somo la Information Technology (IT) katika ngazi ya msingi kwa muktadha wa kukabiliana na maboresho ya mtaala mpya.

(b) Ni lini Wizara yako itazipatia vifaa vya mafunzo ya amali skuli za msingi za Mwanakwerekwe ili kuendana na umahiri wa mabadiliko ya mtaala mpya.

**Wizara ya Afya:**

9. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukuwa katika kuimarisha sekta ya afya nchini kwa kujenga hospitali kubwa na nzuri katika kila Wilaya.

(a) Ni ipi tathmini halisi ya maendeleo ya hospitali hizi.

(b) Ni changamoto zipi Serikali kupitia Wizara yako inaendelea kukumbana nazo katika kutoa huduma kupitia hospitali hizi kwa sasa.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

69. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

(a) Ni tafiti ngapi na zipi zimefanywa kwenye sekta ya maendeleo ya jamii na jinsia mpaka hivi sasa.

(b) Tathmini iko vipi juu ya mabadiliko na miongozo inayotokana na tafiti hizo katika kupunguza vitendo vya ukatili hususani kwa watoto na kinamama wenye mahitaji maalumu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

266. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto omba omba katika eneo la Forodhani na maeneo ya mjini ambao huleta kero kubwa kwa wageni na wenyeji wanaotembelea maeneo hayo yenye vivutio vya utalii katika kisiwa chetu cha Unguja na kuleta taswira mbaya kwa Sekta ya Utalii.

(a) Je, kwa kiwango kipi Serikali inalitambua tatizo hili linalozidi kuongezeka kila siku katika maeneo haya ya vivutio vya utalii.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo la watoto omba omba katika eneo la Forodhani na maeneo ya Mji Mkongwe ili kuboresha mandhari na hali ya usalama kwa wageni.

(c) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuhakikisha watoto hawa wanarejeshwa katika maeneo wanayotoka ambao kwa kiasi kikubwa wanaonekana ni wageni kutoka nje ya Zanzibar.

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**

**Zanzibar,**
**11 Septemba, 2024.**